

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI

DAR ES SALAAM.

MAOMBI YA MAREJEO NA. 545/2019

BAINA YA

JHPIEGO.....APPLICANT

NA

LYDIA TIRWESHOBWA.....RESPONDENT

HUKUMU

Tarehe ya mwisho ya Amri:22/02/2021

Tarehe ya Hukumu:10/03/2021

Z.G.Muruke, J.

Mjibu maombi Lydia Tirweshobwa, aliajiriwa na muombaji katika cheo cha Program Assistant (Msaidizi wa program) mnamo tarehe 16/04/2012. Alifanya kazi mpaka tarehe 17/06/2013 alipoachishwa kwa sababu ya kughushi stakabadhi ya gharama za malazi. Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, mnamo mwezi february, 2013 Bi. Lydia alisafiri kikazi kwenda Bagamoyo ambako alifikia katika hoteli iitwayo Bagamoyo Town Lodge. Inasemekana kwamba katika hoteli hiyo alikaa katika chumba cha gharama ya shilingi 35,000/= lakini katika stakabadhi ya malipo ya gharama hizo ziliaandikwa kiasi cha shilingi 60,000/= Kughushi huko, kuligundulika baada ya mjibu maombi kuwasilisha stakabadhi hizo kwa muombaji na zikatiliwa shaka na muajiri ambaye aliagiza Meneja kwenda

kufanya uchunguzi juu ya gharama hizo katika hoteli hiyo. Tuhumu hizo zilipelekea Mjibu maombi kuachishwa kazi jambo ambalo hakuridhika nalo hivyo kupeleka mgogoro huo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) ambako maamuzi yalikuwa upande wake. Tume iliamuru alipwe fidia ya mishahara ya miezi kumi na mbili(12) kwa kuachishwa kazi isivyo halali. Muombaji hakuridhika na uamuzi huo wa tume, aliwasilisha maombi haya kuomba kutenguliwa kwa uamuzi huo wa tume kwa sababu zilizoainishwa katika aya ya 7,8,9,10 na 11 ya hati ya kiapo cha Mashaka Nyenza Afisa Rasilimali Watu wa muombaji. Maombi hayo yalipingwa na kiapo cha mjibu maombi.

Kwa ridhaa ya mahakama, maombi haya yaliwasilishwa kwa njia ya maandishi. Muombaji aliwakilishwa na wakili Blandina Kihampa, wakati Mjibu maombi aliwakilishwa na Madaraka Ngwiye muwakilishi kutoka CHODAWU.

Katika mawasilisho yake, wakili wa mleta maombi alieleza kwa pamoja sababu ya 7,8,9 kwamba, muamuzi katika kuamua kwake ameshindwa kuzingatia kipimo cha uzito wa ushahidi katika kesi za madai ambacho kiko katika urari wa uwezekano. Katika ushahidi wao DW1 na DW2 wote walithibitisha kuwa mjibu maombi alikuwa na hatia ya kughushi stakabadhi ya malazi, kwa kumuomba maneja wa hoteli ya Bagamoyo Town Lodge kumuandikia stakabadhi ya shilingi 60,000/= ilhali gharama sahihi ya chumba alicholala ni shilingi 35,000/=. Walitoa kielelezo A2 (stakabadhi iliyoghushiwa) lakini muamuzi alitaka risiti iliyoonyesha gharama sahihi na mashahidi walioshuhudia kughushi huko, jambo ambalo

si sahihi kwasababu risiti iliyotolewa ni hiyo iliyokuwa na gharama zisizo sahihi iliyotolewa kwa maelekezo ya mjibu maombi. Wakili alieleza zaidi kuwa katika urari wa uwezekano, kuna uwezekano mkubwa kuwa mjibu maombi alifanya kosa hilo lakini muamuzi alishindwa kutumia kipimo hicho na kufikia maamuzi yasiyo sahihi.

Katika sababu ya 10 na 11 kwa pamoja, Wakili Blandina Kihampa alieleza kuwa, fidia ya kuachishwa kazi hutolewa tu pale kunapokua na uachishwaji kazi usio halali. Muombaji alikuwa na sababu ya msingi ya kumuachisha kazi mjibu maombi hivyo hakustahili fidia ya miezi kumi na mbili (12) iliyotolewa na Muamuzi. Pia ni misingi ya kisheria kwamba, mtu anapoachishwa kazi kwa makosa ya utovu wa nidhamu, hastahili kulipwa kiinua mgongo. Kutokana na sababu ya muombaji, mjibu maombi hakustahili kulipwa kiinua mgongo kama alivyoamrisha muamuzi. Wakili alimalizia kwa kueleza kuwa mjibu maombi aliachishwa kazi kihalali kabisa, hivyo uamuzi wa tume hauna mantiki hivyo aliomba ufanyiwe marejeo na kutenguliwa.

Kwa upande wa mjibu maombi Bwana Madaraka katika sababu ya 7,8 na 9 kwa pamoja alieleza kwamba, tume ilizingatia ushahidi uliotolewa na pande zote mbili na kuzingatia uzito wa ushahidi katika kufikia uamuzi wake huo.

Kuhusiana na sababu ya 10 na 11 muwakilishi wa mjibu maombi alieleza kwamba, tume ilikuwa sahihi kumuamuru muombaji kumlipa mjibu maombi fidia ya miezi kumi na mbili pamoja na kiinua mgongo kwasababu, Muombaji ameshindwa kuthibitisha sababu ya kumuachisha kazi mjibu

maombi, alirejea kifungu cha 40(1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 (hapa itajulikana kama Sura ya 366 Marejeo ya 2019)

Baada ya kupitia maelezo ya pande zote mbili, Mahakama ina hoja zifuatazo za kujiuliza:

- i. **Iwapo Muombaji alikuwa na sababu ya msingi ya kumuachisha kazi mjibu maombi na kama taratibu zilifuatwa.**
- ii. **Zipi ni stahiki za wadaawa.**

Katika kujibu hoja ya kwanza, ni matakwa ya kisheria kwamba ili kuachishwa kazi kuwe halali, ni lazima muajiri athibitise kuwa sababu ni halali na ya haki na pia uachishwaji huo umefuata taratibu zilizoainishwa kisheria, kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 37(2) cha Sura ya 366 Marejeo ya 2019. Kifungu hicho kimeeleza:

'Section 37 (2) A termination of employment by an employer is unfair if the employer fails to prove:-

- (a) that the reason for the termination is valid;*
- (b) that the reason is a fair reason:-*
 - (i) related to the employee's conduct, capacity or compatibility; or*
 - (ii) based on the operational requirements of the employer, and*
 - (c) that the employment was terminated in accordance with a fair procedure."*

Mahakama hii katika shauri la **National Microfinance Bank V. Japhet Machumu**, Rev. No. 710/2018 (unreported) iliamua kwamba:-

"Termination of employment must be first substantively fair with fair and valid reasons putting in regard that the concept of right to work as a component of human rights, is so fundamental..."

Mleta maombi alieleza kuwa kosa aliloshtakiwa nalo mjibu maombi ni kughushi gharama za malazi na kuwa, muamuzi ameshindwa kuangalia uzito wa ushahidi uliotolewa na DW1 na DW2 ambao ulitosha kuthibitisha shtaka dhidi ya mjibu maombi. Tume iliona kwamba mleta maombi alishindwa kuthibitisha shtaka dhidi ya mjibu maombi.

Baada ya kupitia kumbukumbu za shauri hili, niwazi kuwa ushahidi pekee uliopo ni wa DW1 ambaye ndiye aliyefanya uchunguzi wa tuhuma hizo ambaye alitoa vielelezo viwili vya gharama za usafiri (kielelezo D1) na stakabadhii iliyoghushiwa (kielelezo D2). Katika kumbukumbu, hakuna ushahidi uliotolewa na mtu kutoka katika hoteli hiyo aidha katika tume au kikao cha nidhamu. Kilichoelezwa ni maneno ambayo DW1 anaiaminisha mahakama kuwa yalitokana na maelezo ya meneja wa hoteli hiyo kwamba bei halisi ya chumba alicholala mjibu maombi ni shilingi 35,000/= na sio 60,000/=. Mahakama hii ilitegemea kwamba, baada ya yeye DW1 kwenda kufanya uchunguzi hapo katika hoteli aliyolala mjibu maombi, angekuwa na kielelezo kingine kitakacho thibitisha maelezo ya meneja wa hoteli hiyo na tuhuma dhidi ya mjibu maombi mfano, nakala ya kitabu cha wageni ambacho kingeonyesha kwa siku za nyuma chumba alicholala mjibu maombi kililipiwa kiasi gani na wateja wengine. Ushahidi uliotolewa hauna nguvu ya kuthibitisha tuhuma dhidi ya mjibu maombi pamoja na kwamba uzani wa ushahidi katika mashauri ya madai ni katika urari wa uwezekano. Muamuzi alikuwa sahihi katika kuona kwamba mleta maombi

ameshindwa kuthibitisha tuhuma dhidi ya mjibu maombi hivyo hana sababu halali ya kumuachisha kazi mjibu maombi.

Katika hoja ya pili, mleta maombi ameeleza kwamba, muamuzi hakuwa sahihi kwa kumuamuru amlipe mjibu maombi fidia ya miezi kumi na mbili(12). Kama alivyoeleza wakili wa mleta maombi mwenyewe kwamba fidia hutolewa tu pale uachishwaji kazi unapokua sio halali. Hili limeelezwa katika kifungu cha 40(1) (c) la Sura ya 366 Marejeo ya 2019 kwamba:

**'40.-(1) If an arbitrator or Labour Court finds a termination is unfair, the arbitrator or Court may order the employer-
(c) to pay compensation to the employee of not less than twelve months' remuneration.**

Katika shauri hili ni wazi kuwa mleta maombi hakuwa na sababu ya msingi ya kumuachisha kazi mjibu maombi kama ilivyoamuriwa hapo juu. Hivyo basi uachishwaji wa mjibu maombi ulikuwa sio wa haki, kwa hiyo basi sioni sababu ya kutengua amri hiyo ya tume juu ya fidia ya mjibu maombi.

Hivyo basi, kwa kuzingatia sababu zilizojadiliwa katika hukumu hii, maombi haya ya marejeo yanatupiliwa mbali kwa kukosa mashiko. Imeamriwa hivyo.


Z.G. Muruke

JAJI

10/03/2021

Hukumu imesomwa leo mbele ya Pray God Uiso, Wakili akishika mikoba ya Blandina Kihampa na Madaraka Ngwije mwakilishi wa mjibu maombi.



Z.G. Muruke

JAJI

10/03/2021

Labour Court TZ.